



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**VYAMA VYA SIASA NA WAGOMBEA KUZINGATIA SHERIA,
KANUNI NA MAADILI YA UCHAGUZI**

Kwa mujibu wa Ibara ya 74 (6) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, inawakumbusha Viongozi wa Vyama vya Siasa na Wagombea kuendelea kufanya Kampeni zao kwa kuzingatia Katiba, Sheria, Kanuni na Maadili ya Uchaguzi katika muda wote wa Kampeni uliosalia mpaka kufikia siku ya Kupiga Kura.

Aidha, Tume inawasisitiza Viongozi wa Vyama vya Siasa na Wagombea kufanya Kampeni kwa kuzingatia misingi inayolenga kutangaza Sera za Vyama vyao ambazo hazijengi chuki, mfarakano wala mgawanyiko katika jamii. Viongozi wa Vyama vya Siasa na Wagombea wajenge mazingira ambayo yatawezesha Uchaguzi kufanyika kwa Uhuru, Haki na Amani.

Imetolewa na;

Hamis A. Mkunga

KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI

17 Januari 2017